The Project is funded by the European Union

Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

# KIJARIDA CHA MRADI WA KUONGEZA THAMANI KATIKA MISITU YA MILIMA YA TAO LA MASHARIKI (AVA)

*Kimechapishwa Machi 2015*


## AVA NINI?

AVA ni mradi wa kuongeza thamani katika Misitu ya Tao la Mashariki *(Adding Value to the Arc*)

Mradi unafadhiliwa na Umoja wa nchi za Ulaya kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2013 hadi 2017.

Lengo ni kupunguza umasikini na kuboresha shughuli za kiuchumi kwa jamii zinazoishi kando kando ya misitu zinazotegemea rasilimali zinazotokana na misitu na zinategemea rasilimali zinazotokana na misitu iliyoko wilaya ya Mvomero.

Mradi unatekelezwa kwenye vijiji 34 vilivyo kando kando ya Msitu wa Hifadhi wa Kanga na Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Mkingu, ambayo misitu hii ni chanzo muhimu cha maji na sehemu ambapo kuna wanyama na mimea ya kipekee.




*Ramani inayoonyesha vijiji vya mradi*

## MATARAJIO YA MRADI

1. Usimamizi shirikishi wa misitu ya jamii.
2. Usimamizi shirikishi wa misitu ya pamoja.
3. Kuibua miradi rafiki na mazingira kwa ajili ya kuongeza kipato kwa wanajamii.
4. Kujenga uwezo na kuimarisha utawala bora.
5. Ufuatiliaji na upashanaji wa habari kuhusu maendeleo ya mradi.

## MRADI UMEFANYA NINI KWA KIPINDI CHA JULAI 2014 HADI DISEMBA 2014?

### USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISITU YA JAMII

- ✓ Kutambulisha na kujenga uelewa juu mradi kwenye vijiji vya Usimamiazi wa misitu ya jamii.
- ✓ Kuwezesha jamii kuanzisha na kusimamia misitu ya kijiji.
- ✓ Mkutano baina ya kamati ya uvunaji ya wilaya na wanajamii wanaosimamia misitu yao.
- ✓ Kuwezesha jamii kujenga majiko banifu.
- ✓ Kuwaelezea jamii umuhimu wa MKUHUMI.

### USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISTU WA PAMOJA

- ✓ Kutambulisha na kujenga uelewa juu ya mradi kwenye vijiji vya Usimamizi wa Pamoja.
- ✓ Kuunda kamati za maliasili za vijiji.

*JI ULIZE MKO WANGAPI? TULIZANA, BAKI NJIA KUU MCHEPUKO SIYO DILI*

**MIRADI RAFIKI NA MAZINGIRA KWA AJILI YA KUONGEZA KIPATO**

- ✓ Vikundi 20 vya wa kulima wa kilimo hifadhi vimeanzishwa.
- ✓ Safari ya mafunzo ya kilimo hifadhi.
- ✓ Utafiti wa kitaalamu kuhusu kilimo hifadhi.
- ✓ Kuimarisha vikundi vya hisa.
- ✓ Majiko banifu

**KUJENGA UWEZO NA KUIMARISHA TAASISI ZA SERIKALI KATIKA KUTEKELEZA USIMAMIZI WA MISITU**

- ✓ Safari ya mafunzo wa wataalam
- ✓ Elimu ya mazingira kwa walimu wa shule za msingi.
- ✓ Kubainisha maeneo ya utalii kwenye hifadhi ya mazingira Asilia ya Mkingu.

**UFUATILIAJI NA UPASHANAJI WA HABARI**

- ✓ Taarifa malimbali za mradi zimetangazwa kwenye Radio ya Abbod na TV.

## USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISITU YA JAMII (USMJ)

Wanakijiji wa kijiji cha Makuyu, Msolokelo na Masimba walielezwa faida zitokanazo na Usimamamizi Shirikikishi wa Misitu ya Jamii. Faida hizo ni pamoja na Kumiliki Msitu kama mali ya kijiji, wanaweza kutumia rasilimali za msitu mfano mbao, mkaa, kuni, matunda, dawa za miti shamba, kuni kwa njia endelevu. Nje ya faida hizo jamii watakao tenga Misitu mikubwa kama hekta 1000 watanufaika na motisha unaotokana na program ya MKUHUMI. Vijiji vimeandaa mpango wa huvunaji endelevu wa rasilimali za misitu.

**MKUHUMI** ni Mpango wa kupunguza Uzalishaji wa Hewa ya Ukaa kutokana na Ukataji na Uharibifu wa Misitu.

Mpango huu unaoezesha nchi zinazoendelea kutoa motisha ya kifedha kwa jamii zinazohifadhi misitu yao kwa njia endelevu.

Lazima kuwenajuhudi za uhifadhi ndipo motisha utapatikana

Baada ya Jamii ya Makuyu, Msolokelo na Masimba kuelezwa faida hizo walikubaliana na kuweza kutenga maeneo ya Misitu ya kijiji. Misitu hii itakuwa ni Misitu ya Hifadhi ya kijiji. Ukubwa wa misitu iliyotengwa ni hekta 5,310.95 (Msolokelo hekta 1574.24, Makuyu hekta 578.1 na Masimba hekta 3158.61). Pia waliandaa mpango endelevu wa uvunaji. Kijiji cha Makuyu akitaweza kunufaika na MKUHUMI kwa kuwa eneo walilotenga ni dogo alifikii hekta 1000.

## KUJENGEA UWEZO WATAALAM

Kujifunza ni sehemu ya kuimarisha utelezaji wa shughuli za Mradi wa AVA. Mradi uliandaa safari ya mafunzo kwa wadau wanaotekeleza mradi (H/W Mvomero, Wakala wa Huduma za Misitu na watumishi wa mradi). Wataalam walijifunza jinsia ya kufikia malengo ya mradi na kukabiliana na changamoto. Wataalam walitembelea mkoa wa Tanga katika Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Amani, Manyara shirika la farm Africa na msitu wa Boreko, Singida vikundi bora vya wafugaji nyuki.

## USIMAMIZI WA PAMOJA WA MSITU (UPM)

Ni miaka mingi tokea serikali ya Tanzania ianze mchakato wa kushirikisha jamii kuhifadhi misitu ya serikali pamoja na wananchi. Shughuli moja wapo ya Mradi wa AVA  Mradi ni kushirikiana na wakala wa huduma za Misitu kuwawezesha wanajamii waliozunguka msitu wa Hifadhi ya Mlima Kanga na Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Mkingu wanashiriki na kunufaika na uhifadhi huu. Kwa kipindi hiki cha miezi sita mradi umeamasisha vijiji 16 (Digalama, Digoma, Komtonga, Mlaguzi, Kinda, Makate, Semwali, Dibago, Maskati, Pemba, Gonja, Kwelikweji, Mafuta, Ubiri, Mndela na Kisimaguru) kwa njia ya mikutano na vipeperushi.

Afisa Misitu kutoka Mkingu alielezea kwa undani  faida zitakazotokana na usimamizi wa pamoja wa msitu wa Mkingu. Moja wapo ya  faida/mapato yatakayokuwa yanaingia kwenye hifadhi yatagawanywa kwa asilimia kwa mujibu wa muongozo wa usimamizi shirikishi wa pamoja uliotolewa mwaka 2013. Mgawanyo huo utakuwa 46% ya mapato yatokanayo na  hewa ya ukaa kama mpango huu utatekelezeka Tanzania,  32% ya mapato yatokanayo na faini, 36% ya mapato yatokanayo na tafiti, ada ya viingilio, sehemu za kuweka mahema na minara ya simu, 26% mapato yatokanayo na utalii na 49%ya mapato yatokanayo na mazao ya msitu yaliyokamatwa na kutaifishwa. Licha ya mgao wa mapato kunafaida nyingine wanajamii wanaweza kuzipata kwa utaratibu maalum bila kuharibu mazingira; faida hizo ni ukusanyaji wa kuni, madawa ya miti shamba, mbogamboga, uyoga, matunda, maji na nyasi za kuezekea.

Hata hivyo ili haya yote yaweze kutimia ni lazima kuwe na makubaliano kati ya serikali/TFS na Halmashauri za vijiji jinsi ya kusimamia misitu hii, pia kila upande utekeleze majukumu yake ipasavyo.

*Wananchi wa kijiji cha Maskati wa kizindua mradi wa AVA*



*wanakijiji wakifurahia uzinduzi wa mradi wa AVA*

## SAFARI YA MAFUNZO KWA WAKULIMA

Kilimo ndio uti wa mgongo wa Taifa la Tanzania, asilimia 98 ya watanzania wote wanategemea kilimo. lakini wengi wao kilimo wanachotumia sio kile ambacho kinaweza kubadilisha maisha yao na kulinda mazingira. Mradi kwa kuwa unalengo la kupunguza umasikini kwa jamii zinazoishi kandolando ya msitu. Mradi umeandaa washauri wa kitaalamu ambao wanafanya tafiti na kufundisha wakulima juu ya kilimo hifadhi. Pia mradi umewapeleka wakulima 28 kwenye kituo cha utafiti wa kilimo cha Seliani Arusha (*SARI).* Kwa ajili ya mafunzo.

## MAFUNZO YA MAJIKO BANIFU

Ili kupunguza utegemezi mkubwa wa misitu kwa ajili ya kuni, na kupunguza ugumu wa maisha kwa wanajamii wanao nunua kuni (fungu shilingi 2000 hadi 3000) upatikanaji wa kuni kwa ajili ya kupikia mradi umeanza kuwawezesha wanajamii kutengeneza. Pia majiko haya yanapunguza muda wa kukusanya kuni hivyo kuweza kutumia muda huo kwa shughuli nyingine za kimaendeleo, Mradi umetoa mafunzo ya kutengeneza majiko banifu yanayotumia kuni chache kwa wanawake wanamtandao wa MJUMITA. Mitandao iliyoanza kupata

mafunzo ni TUMIM (Kata ya Mhonda), JUWAMIPE (Kata ya Pemba), HIMIDI (Kata ya Diongoya) na HIMAYAKA (Kata ya Kanga). Katika zoezi hili jumla ya wanamtandao 53 walijifunza na kutengeneza majiko.



*Mama akitengeneza jiko banifu*

## MAFUNZO KWA KAMATI YA MALIASILI YA KIJIJI

Misitu ya kijiji na ile ya usimamizi wa pamoja itaweza kupona kama wanajamii wataajibika kwa pamojo wakishirikiana na serikali na Kamati za maliasili za vijiji mradi umeona njia moja wapo ni kuwapa elimu ya utawala bora, majukumu ya kamati za maliasili na majukumu ya serikali ya kijjiji juu ya usimamizi wa misitu. Kwa kipindi hiki Mradi umetoa mafunzo kwa vijiji 3 (Msolokelo,Makuyu, Masimba) ambavyo vinatekeleza Usimamizi shirikishi wa misitu ya Jamii.

## MAFUNZO YA ELIMU YA MAZINGIRA KWA WALIMU WA SHULE ZA MSINGI

Kuna usemi usemao mtoto umleavyo ndivyo akuwavyo. Mradi wa AVA unaamini kwa usemi huu pia, kwahiyo ilikuwajenga watoto wanaoishi kandokando ya mistu. Mradi umetoa mafunzo kwa walimu 22 kutoka shule 22 za msingi, waratibu wa elimu kata 8, mkaguzi wa shule za msingi wilaya na afisa elimu wilaya walipewa elimu ya mazingira na jinsi ya kuweza kufundisha wanafunzi elimu ya mazingira mashuleni na jinsi ya kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi kutokana na elimu ya mazingira aliyoipata.

## MAFUNZO YA KUIMARISHA VIKUNDI VYA HISA

Njia mojawapo ya kumwezesha mwanajamii kiuchumi ni kumwezesha kuweza kutunza kile kidogo anachokipata. Kwa kuzingatia hilo mradi umefanikiwa kutoa elimu kwenye vikundi vya Hisa vipatavyo 21. Wanajamii walioshiriki katika mafunzo ni 593 (wanawake 321 (54%) na wanaume ni 272 (46%).


**KWA MAWASILIANO ZAIDI**

***Mkurugenzi Mtendaji TFCG: S.L.P 23410, Dar es Salaam, Simu: +255 22 2669007,Barua pepe: tfcg@tfcg.or.tz/www.tfcg.org***

***Mkurugenzi Mtendaji MJUMITA: S.L.P 21522, Dar es Salaam, Simu: +255 22 2669007***

***Kwa wanajamii ya Wilaya ya Mvomero wanaweza kuwasiliana na Meneja wa mradi Ndugu Hassan ChikiraKwa namba zifutazo: Simu yamkononi: 0782217846 au 0715546448***

***Au***
***Fika kwenye ofisi za AVA Madizini B***